**MJAWA SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 50,KIBITI- COAST Tel: +255 620 194 418**
**E_mail: sekondariyamjawa12@gmail.com**

Kumb. Na MJSS/F1/2021

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi______________________________________________________

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE**

1. Ninayo furaha kukujulisha kuwa kijana wako __________________________________ amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari Mjawa mwaka 2021. Shule yetu iko kijjii cha Mjawa Wilaya ya Kibiti Mkoa wa Pwani, ni shule ya kutwa na mchanganyiko (Wavulana na Wasichana) muhula wa masomo utaanza Tarehe____________. Unatakiwa kumleta shuleni tarehe____________ na mwisho wa kuripoti ni tarehe ____________ Iwapo kijana wako hatofika shuleni hadi tarehe ____________ hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako.

**2. MAMBO YA MUHIMU YA KUZINGATIWA.**

**2.1 SARE YA SHULE**

(a) Kwa wavulana ni:

i. Suruali 02 rangi nyeusi (isiwe modo /mdomo wa chupa
ii. Mashati mawili mikono mifupi meupe.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi jozi 02
iv. Soksi nyeusi jozi 02
v. Mkanda mweusi
vi. Bukta rangi ya bluu kwa ajili ya michezo
vii. Raba rangi nyeupe kwa ajili ya michezo
viii. T-shirt ya rangi ya bluu kwa ajili ya michezo

(b) Kwa wasichana :

i. Sketi mbili nyeusi mshono wa linda boksi ziwe ndefu kuvuka magoti
ii. Viatu vyeusi vya ngozi visiwe na visigino virefu
iii. Raba rangi nyeupe kwa ajili ya michezo/track suit 02 kwa ajili ya michezo
iv. Soksi nyeupe jozi mbili
v. Mashati meupe mikono mifupi au nusu kanzu itakayovaliwa na hijabu jozi 02.

**3. MAHITAJI YA DARASANI**

i. Madaftari makubwa (Counter book) au daftari zenye kurasa 80 ziwe kumi.
ii. Mkebe wa Hisabati
iii. Kamusi ya kiingereza na Kiswahili (Dictionary)
iv. Begi la kubebea madaftari
v. Kalamu za wino wa blue/nyeusi na penseli za kutosha

MJAWA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 50,KIBITI- COAST Tel: +255 620 194 418
E_mail: sekondariyamjawa12@gmail.com

**4. MAMBO MENGINE**

I. Mwanafunzi aje na fagio ya chelewa ya wima

II. Mwanafunzi anatakiwa kuleta kiti na meza *( rejea kikao cha wazazi tarehe 17/12/2020)*

**5. UTORO/UJAUZITO KWA MWANAFUNZI**

Pamoja na operesheni kubwa kitaifa, tumejipanga pia na kuthibiti utoro/ujauzito kwa utaratibu maalum;

- Kwa utoro wa jumla wa majuma 02, mwanafunzi ataitwa na mzazi/mlezi wake mbele ya kamati ya Nidhamu/Mkuu wa shule
- Utoro wa jumla ya majuma 04, mwanafunzi ataitwa na mzazi/mlezi wake mbele ya Kamati ya Bodi ya Shule
- Utoro wa zaidi ya majuma 04 mwanafunzi na mlezi/mzazi wake wataitwa mbele ya Afisa Mtendaji Kata kwa ajili ya kufikishwa mahakamani.
    - ❖ Tafadhali sana, kuwa makini na maelezo/maelekezo haya na kuyatekeleza
    - ❖ Vifaa vilivyoagizwa vitakaguliwa siku ya kuripoti

Motto wa Shule yetu ni **Fanya Vizuri Zaidi** *(Do the Best)*

KARIBU SANA!!

________

NGOZI, A. C

**MKUU WA SHULE**

MJAWA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 50,KIBITI- COAST Tel: +255 620 194 418
E_mail: sekondariyamjawa12@gmail.com

**SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA KUZINGATIA UWAPO SHULENI NA NJE YA SHULE**

1. Unapokuwa eneo la shule; vaa sare za shule, sare za michezo kwa siku za michezo (**shati jeupe la mikono mifupi**[*lililochomekewa muda wote*]**sketi/suruali nyeusi**) na **t-shirt za blue [***zenye nembo ya shule*] zisizobana, **kiatu cheusi** [cha kamba, kisicho na madoido; raba na ‘boots’ si sehemu ya sare) na soksi (*wasichana nyeupe/wavulana nyeusi)*
2. Unatakiwa kuongea Kiingereza wakati wote uwapo shuleni.
3. Kutii kengele inapogongwa na kufika eneo husika kwa haraka
4. Fuata ratiba kwa kuhudhuria unakotakiwa kwa wakati.
5. Kuwahi shule tarehe husika ya kufungua shule, na saa moja kamili asubuhi kila siku za wiki, zaidi ya hapo utahesabika mchelewaji.
6. Huruhusiwi kuondoka kabla ya muda ama kuwa mbali na eneo la shule muda wa masomo na wakati wa mapumziko mafupimafupi, isipokuwa kwa ruhusa maalum (*utapewa pass)*
7. Sharti kuheshimuWimbo waTaifa na Bendera yaTaifa.
8. Ni MARUFUKU kufuga ndevu/sharubu, nywele, kupaka kucha rangi/hina kwenye kucha/midomo, kuchonga nyusi, kuvaa hereni, kunyoa kihuni (kiduku, kipara cha wembe, panki, n.k)
9. Ni MARUFUKU kuvuta sigara, tumbaku, kubwia ugoro, kunywa pombe au kutumia kilevi cha aina yoyote, kuingia vilabu vya pombe, nyumba za wageni (guest house)
10. Heshimu walimu, wafanyakazi, viongozi (*viranja, viongozi wa madarasa)* wageni, shuleni na nje ya shule (*wapokee mizigo)*.
11. Kuwajibika katika shughuli zote za kishule; **Kitaaluma**, **kazi za mikono** na shughuli za **kimichezo.**
12. Onesha ushirikiano baina ya wanafunzi na walimu.
13. Tunza vifaa na mali za shule
14. Si ruksa kuchukua mali za shule yakiwemo mazao bila ruhusa ya mwalimu mwenye dhamana.
15. Kuwa nadhifu wakati wote (usafi wa mwili , mavazi, na mazingira, madarasa, viwanja vya michezo na kutunza bustani.
16. Hurusiwi kumiliki simu, radio, wala kamera uwapo shule.
17. Ruhusa/taarifa ya ugonjwa, dharura inaombwa/kutolewa na mzazi/mlezi wa mwanafunzi husika.

**Makosa yanayoweza kusababisha kusimamishwa/kufukuzwa shule:**

**i.** Kudharau Bendera ya taifa au wimbo wa Taifa na alama nyingine za Taifa.
**ii.** Kupigana au kupiga(ugomvi)
**iii.** Kudharau uongozi wa shule, walimu na viongozi wa wanafunzi
**iv.** Kukataa au kugomea adhabu
**v.** Kutukana, Wizi, Ubakaji
**vi.** Uasherati na ushoga
**vii.** Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, sigara, kuberi, cocaine n.k
**viii.** Kusababisha, kupata au kutoa mimba
**ix.** Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
**x.** Kuoa au kuolewa
**xi.** Kumiliki na kutumia simu ya mkononi, radio na kamera shuleni.
**xii.** Utoro sugu
**xiii.** Kuchochea, kugoma na kuongoza mgomo au kushiriki kuvuruga amani na usalama was hule au watu wengine
**xiv.** Makosa ya jinai

***TII SHERIA BILA SHURUTI KWA MAENDELEO YA SHULE YETU!***

MJAWA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 50,KIBITI- COAST Tel: +255 620 194 418
E_mail: sekondariyamjawa12@gmail.com

**FOMU YA KUKIRI/KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE**

Mimi ________________________________________ mzazi/mlezi wa mwanafunzi __________________ wa Kidato cha ______________ katika Shule ya Sekondari Mjawa, ninakiri kwamba nimesoma na kuelewa maelekezo ya shule na nathibitisha kuwa nipo tayari kuyafuata kikamilifu kama nitakavyoelekezwa na Uongozi wa shule, Bodi ya Shule au Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti kwa maendeleo ya shule na mwanafunzi. Hii ni pamoja na upatikanaji wa huduma zote anazotakiwa kuzipata.

S. L. P ___________, Kitongoji cha ____________, Kijiji cha __________, Kata ya ________ Tarafa __________, Simu _________________ Saini ______________________________

Mimi _________________________, mwanafunzi NAKUBALI/SIKUBALI (*kata isiyohusika*) nafasi hii niliyopewa na serikali/taifa kusoma katika shule hii. Naahidi kujifunza masomo yote kwa bidii na kufanya mitihani yote na kwamba nitakuwa mwaminifu na mvumilivu, sitakuwa mtoro wala mdanganyifu kwa muda wote na mahali popote, pia nitafuata sheria na taratibu za shule kama nitakavyoelekezwa na uongozi wa shule .

Mgomo au maandamano kwangu mwiko!

Jina la Mwanafunzi ________________________________________

Tarehe ______________ Saini ___________________

**KIAMBATANISHO ‘C’: USAJILI**

*(IjazwenakukabidhiwaOfisiyaMsajiliShuleni)*

Jina Kamili la Mwanafunzi: ____________________________
Tarehe ya Kuzaliwa: ____________________________
Mahali alipozaliwa: ____________________________
Uraia: ____________________________
Shule ya Msingi alipomaliza: ____________________________
Dini yake: ____________________________

Jina la Mzazi/Mlezi: ____________________________

Kazi ya Mzazi/Mlezi: ___________________
Anuani yake: ___________________
Namba ya simu: ___________________

*(Mabadiliko yoyote mawasiliano hapo juu yawasilishwe shuleni mara moja )*

Majina ya Ndugu/Jamaa wa Karibu na mawasiliano yao

| Na. | Jina | Uhusiano | Anuani/Simu |
|---|---|---|---|
| 01. | | | |
| 02. | | | |

MJAWA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 50,KIBITI- COAST Tel: +255 620 194 418
E_mail: sekondariyamjawa12@gmail.com

## *REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION*

To: THE MEDICAL OFFICER,

____________________
____________________
____________________
____________________

Please examine ………………………………………………….

As his/her fitness as a student in the following areas:-

1. Eye sight ………………………………………………….
2. Hearing ………………………………………………….
3. Speech ………………………………………………….
4. Specimen …………………………………………………..
    i. Stool ………………………………………………….
    ii. Urine ………………………………………………….
    iii. Blood ………………………………………………….
5. Asthma ………………………………………………….
6. T. B …………………………………………………………..
7. Pregnancy (for girls) ………………………………………………….
8. Other diseases …………………………………………………………
9. Any disability reported ………………………………………………….
10. Hereditary diseases especially Diabetes/ Epileptic ……………………………

**MEDICAL CERTIFICATION:**

Ihave examined the above mention student and found that he/she is physically fit/unfit as a student.

Signature: ……………… Station………………………………

Designation: ……………… Date: ………………………………

Note: At the examination please treat the individual for any illness noted.